

Heri taifa alilochaguwa Bwana

Zab32,4-5,6-9,18-20 na 21-22.

Siku ya Mungu ya Utatu Mtakatifu, Mwaka B

Musique: Grace Mushagalusa Fabrice

R/He - ri - ta - i - fa-a - li-lo-cha-gu - a - Bwa - na - ku - wa-u - ri - si - wa - ke

9

1. Neno la Bwana ni la kweli,
matendo yake yote ni maaminifu.
Anapenda unyofu na haki:
dunia imeja wema wake Bwana.
2. Mbingu zimefanyiwa kwa neno la Bwana,
na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.
Maana yeye alisema, vikawa;
yeye aliamuru, vikawapo.
3. Macho ya Bwana yawaelekeya wanaomheshimu,
wale wanaotumainia wema wake.
Roho yetu inamngojea Bwana,
yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu.
4. Kweli moyo wetu unafurahiwa kwake,
twategemea jina lake takatif.
Huruma yako, ee Bwana, itushukiye,
kama vile tunavyokutumainnia.